# COVID-19

ONE ALBUQUERQUE city of albuquerque

Jiji la Albuquerque lipo kwa ajili yako wakati huu wa kilele cha janga hili. Nyenzo zilizopo hapa chini zinapatikana kwa wakazi wote wa Albuquerque. Taarifa zinaweza kufikiwa kwa lugha 140. Piga simu 311 ili kuunganishwa na nyenzo humu Jijini.

## Nilipoteza kazi yangu kutokana na COVID-19, je, nitawezaje kulipa bili zangu?

**MANUFAA KWA WASIO NA KAZI:**

Jimbo la New Mexico linahakikisha kwamba bima kwa wasio na kazi (malipo ya kila wiki) inapatikana kwa watu ambao wameachishwa kazi, hawana kazi, au hawaitwi wafanye kazi za kutumikishwa majumbani, mikahawani, na biashara nyingine zilizoathiriwa na virusi vya korona. New Mexico inaondoa lile sharti kwamba watu wasio na kazi (au watu ambao wanaachishwa kazi sasa au ambao hawaitwi kazini ili wafanye kazi kwa saa) wanapaswa kutafuta kazi ili kupata manufaa. Unaweza kuomba manufaa haya kwenye NM.gov

**MSAADA WA MASUALA YA KODI:**

Kufukuzwa kwenye nyumba kutokana na kushindwa kulipa kodi (ikiwemo majengo yanayomilikiwa na watu binafsi) kumesimamishwa kwa muda mfupi kote jimboni katika kipindi hiki cha dharura ya janga la umma la COVID-19. Endapo mwenye nyumba atafungua kesi ya kumfukuza mpangaji, mpangaji huyo atapokea hati ya kuitwa shaurini inayomjulisha kuhusu kesi hiyo na inayoeleza kwamba anaweza kushiriki kusikiliza kesi hiyo mbele ya Jaji. Usikilizaji wa kesi za kortini huendeshwa kupitia video au simu katika kipindi hiki cha dharura ya afya ya umma, isipokuwa kama wahusika wameomba wafike mahakamani ana kwa ana. Ili kuzuia kufukuzwa kwa mpangaji, wapangaji- iwe ardhi kwenye kiwanja kwa nyumba zinazohamishika au fleti - lazima washiriki wakati wa kusikiliza kesi na kumpa Jaji ushahidi unaoonyesha kwamba hawawezi kulipa kodi yao kwa sasa. Endapo ushahidi wa kutosha ukitolewa na mpangaji, majaji watasimamisha amri ya kumfukuza mpangaji ambayo wamiliki wanaweza kupata na kuwapa washurutishaji sheria ili kumuondoa mpangaji kwa nguvu.

**Ikiwa ungependa usaidiwe kwa kesi yako ya kutaka kufukuzwa tafadhali wasiliana na:**

- Msaada wa Kisheria New Mexico - 1-833-LGL-HELP (1-833-545-4357).
- Ofisi ya Sheria ya Raia Wazee - (505) 265-2300, (Huwa inahudumia wakazi wa kaunti za Bernalillo, Sandoval, Valencia na Torrance ambao wana umri wa miaka 60 au zaidi.)
- Mpango wa Nyenzo za Kisheria kwa Wazee, 800-876-6657 jimboni kote; 505-797-6005 kwa Albuquerque, (Namba ya Msaada wa kisheria wa bure ya Jimbo zima ya wakazi wa NM wenye umri wa miaka 55 na zaidi.)

**Mashirika Yanayosaidia watu Kupata Makazi**

- All Faiths Safehouse: 505-271-0329
- Barrett House: 505-243-4887
- Family Promise: 505-268-0331
- Joy Junction: 505-877-6967
- New Mexico Coalition to End Homelessness: 505-217-9570

**Ikiwa unahitaji usaidiwe kulipa kodi au kupata huduma za jamii, wasiliana na mojawapo ya vituo vifuatavyo vya Afya na Huduma ya Jamii:**

- Alamosa Health & Social Service Center - (505) 836-8800 - 6900 Gonzales SW, Albuquerque, NM 87121
- Los Griegos Health & Social Service Center - (505) 761-4050 - 1231 Candelaria NW, Albuquerque, NM 87107
- John Marshall Health & Social Service Center - (505) 848-1345 - 1500 Walter SE, Albuquerque, NM 87102
- East Central Health & Social Service Center - (505) 767-5700 - 7525 Zuni SE, Albuquerque, NM 87108

**MSAADA WA CHAKULA:**

- Maeneo ya Chakula ya Shule za Umma za Albuquerque
  - Saa za Kazi: Saa 11 asubuhi – 1 mchana siku za Jumatatu, Jumatano, na Ijumaa tu.
  - Wanafunzi watapata milo kwa siku mbili.
  - Kinapatikana kwa wanafunzi wote wenye umri wa kuenda shuleni walio chini ya miaka 18.
  - Kwa maelezo zaidi ikiwemo maeneo tembelea tovuti https://www.aps.edu/news/coronavirus/aps-identifies-schools-for-student-meal-pick-ups
- Simu-papo ya Chakula kwa Wazee
  - Kama wewe ni mzee na unahitaji vyakula, tafadhali piga simu Idara ya Huduma za Wazee na za Muda Mrefu za New Mexico kwa namba 1-800-432-2080.
- Watoto wa New Mexico
  - Kwa msaada wa utunzaji watoto, vyakula, nepi, nguo, na zaidi.
  - Piga simu kupitia 1-800-691-9067 au tembelea tovuti newmexicokids.org

Kwa maswali au msaada wowote usio na mahusiano na afya, wasiliana na Idara ya Afya ya New Mexico kwa namba 1-833-551-0518.

## Je, watoto wangu watarudi shuleni lini?

Jimbo la New Mexico limeamua kufunga shule zote ili kujaribu kupunguza kasi ya ueneaji wa virusi vya korona. Hii ni muhimu sana kwa sababu hakutakuwepo na matibabu ya kutosha ikiwa kila mtu atakuwa mgonjwa kwa wakati mmoja kwahiyo jaribu kuwaweka watoto wako nyumbani.

Waeleze watoto wako kuwa shule zinafungwa ili kujaribu kupunguza kuenea kwa virusi hivi katika jamii nzima, lakini watoto wengi hawakuwahi kuonyesha dalili mbaya sana kutokana na virusi vya korona. Hii itasaidia watoto wako wasiwaze mno.

## Je, tutapataje intaneti?

Jiji la Albuquerque limehakikisha kwamba wakazi wengi zaidi wanapata intaneti ya bure kwa WiFi (miunganisho pepe ya intaneti) kwa kuongeza maeneo ya ziada ambapo kutotangamana kunawezekana. Hii itasaidia kufikisha intaneti kwa watu wengi iwezekanavyo huku ikiwawezesha wakazi kufuata miongozo ya kutotangamana. Piga simu namba 311 au tembelea http://www.cabq.gov/coronavirus-information/wifi kwa maelezo zaidi.

## Je, haki zangu ni zipi?

Ukikumbana na ubaguzi wowote tafadhali wasiliana na Ofisi ya Haki za Raia: 505-768-4595

## Vipi endapo nahitaji msaada wa ufasiri au ukalimani?

Pigia simu kwa viongozi wa jamii yako ikiwa una maswali au malalamiko yoyote na ili upate msaada wa ukalimani. Ili upate msaada wa ukalimani na ufasiri nje ya jiji la Albuquerque tafadhali wasiliana na:

- Sara Afghani – 505-235-3204 (Dari, Pashto)
- Mohammed Alkwaz – 505-235-1774 (Kiarabu)
- Martin Ndayisenga - 505-225-4344 (Kirundi, Kinyarwanda, Kiswahili, Kifaransa)
- Margarita Galvis – 505-803-8020 (Kihispania)
- Norma Casas – 505-514-5273 (Kihispania)
- Ivette Miramontes – 505-600-1422 (Kihispania)

## Nyenzo za Afya ya Akili

Ikiwa una msongo wa mawazo au una shauku, unaweza kuwasiliana na Kituo cha Agora Crisis Center kwa namba 505-277-3031 au 855-505-4505. Agora ni huduma ya msaada kwa siri yenye washauri nasaha ambao si wataalamu, saa 24 kwa siku/siku 7 za wiki ambao wanaweza kukupa msaada na kukuunganisha na matibabu ya afya ya kitabia kwa Kiingereza. Pia unaweza kupiga simu kupitia 1-866-HELP-1-NM au Mpango wa Afya kwa Wakimbizi kwa namba 505-476-3076.